

**Mwl. Rev. Nahum Williard Malakalinga**, kitaaluma ni Mwalimu wa biashara na uchumi(Bachelor of commerce with education), pia ni mwanatheolojia aliyesoma diploma ya juu ya biblia na teolojia na shahada ya Biblia na teolojia(Advanced diploma in Bible and Theology, and Bachelor Of Bible and Theology). Amekuwa akifundisha masomo ya biashara na uhasibu shule za sekondari Dar-es-Salaam, Mbeya, na Iringa kwa nyakati tofauti tofauti tangu mwaka 2013-2021. Shahada yake ya kwanza aliipata Mwaka 2016 katika chuo kikuu cha ST. JOHN'S UNIVERSITY OF TANZANIA kilichopo Dar-es-Salaam. Shahada yake ya pili ameipata mwaka 2025 katika chuo cha FOUNDATIONS BIBLE TRAINING CENTER kilichopo Georgia-Atlanta-Marekani.

Kwasasa ni mwalimu katika shule ya sekondari Tunduma Tc anaendelea kufundisha wanafunzi pamoja na semina za Neno la Mungu kupitia mialiko mbalimbali ambayo anapewa. Pia ni mratibu wa chuo cha FOUNDATIONS BIBLE TRAINING CENTER-TANZANIA upande wa nyanda za juu kusini.

Hata serikali ya Muungano wa Tanzania ikiamua kuchukua mali zote za matajiri na kuamua kuwagawia watu wote na maskini kwa usawa kitakachotokea baada ya mwaka mmoja ni tajiri kubaki tajiri tena na masikini atabaki kuwa masikini tena. Watu wengi wakipata pesa hukimbilia kununua gari wakidhani tabia ya mtu kuonekana ana pesa ni kuwa na gari, hapana, si kweli, usinunue gari ikiwa bado hujawekeza baadhi ya mali. Wekeza mali nyingi sana kwa sababu zitakupa pesa nyingi ambazo zitakurahisishia kununua gari bila kupata maumivu. Gari itakusaidia kwenye usimamizi wa mali ulizowekeza. Nakushauri uwe na busara unapopata pesa. Ikiwa mshahara wako ndio chanzo pekee cha mapato yako, hiyo ni hatua ya kuelekea umaskini. Weka akiba katika kila mapato na utumie akiba hiyo kuwekeza. Soma kitabu hiki ukurasa hadi ukurasa usiruke, baada ya kukamilika kwa kitabu hicho utapata uzoefu wa kiwango kingine cha maisha yako.

ISBN 978-9912-42-870-6

9 789912 428706

# AKILI ILIYOPONYWA KUHUSU FEDHA



Mwl. Nahum Williard Malakalinga